# VIZUIZI SABA KWA UZIMA WA MILELE.

NA
JOHN WADDEY

Yesu anatueleza ya kuwa njia iendayo mbinguni imesonga na ni yembamba, Mt. 7:14. Neno "imesonga" linatueleza jinsi ilivyojibana na yenye vizuizi kwa roho kufaulu kufika kwenye raha, lazima tushindane kwa bidii kufanya vile vitu vitakavyotupa moyo na kutusaidia na kujitenga na vile vitu vyote vinavyo weza kuzuia safari yetu. Paulo anatusihi sana, *"...Tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu,"* Ebr. 12:1.

Paulo anawasihi wafilipi akisema "*...Ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele. Nakaza mwendo,niifikilie mede ya thawabu ya mwito kuu*, " Fil. 3:13, 14).

Katika karne ya 17 mwalimu mwingereza kwa jina Richard Baxter aliandika kitabu chenye jina, raha ya milele ya watakatifu. Ndani yake alizungumzia "Vizuizi kwenye njia ya mbinguni." Tutayanukulu baadhi ya maneno yake katika mistari ifuatayo.

I**. Kuishi katika dhambi yo yote unayofahamu ni kizuizi**.

Tukitenda dhambi kwa kusudi "*Maana, kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi*," (Ebr. 10:26). Dhambi ya makusudi ni ya kiburi, tunaweza kuomba rehema na kutumainia neema tukikosa bila kujua, lakini kuendelea kutenda dhambi makusudi, ni kukaribisha maafa. Mkristo lazima avifishe viungo vyake katika nchi "*Uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo...ibada ya sanamu...katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani,*" Kol. 3:5-7.

**II. Akili za kidunia huzuia maendeleo, na ni sharti yaepukwe**.

"*........Kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu*," Yakobo 4:4. Yohana anatufundisha , "*msiipende dunia, wala mambo yaliyomo*," 1 Yn. 2:15. Hii inahusu kila aina ya dhambi hapa duniani kama "tamaa ya mwili," "tamaa ya macho" na kiburi cha uzima. Kwa nyongeza anatuonya kutoshikamana kwa tamaa inayozidi kiasi hata kwa vitu safi cya maisha haya. Kama tujuavyo, *"hatukuja na kitu duniani, tena hatuwezi kuondoka na kitu*," 1 Tim. 6:7-9. Wale walio na mawazo ya kuwa tajiri huanguka katika majaribu na mtego na tamaa nyingi za kijinga na za kudhuru, tamaa kama hizo NA zimewavuta wanadamu katika uharibifu kupotea milele, (Mith. 9). "*Shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno likawa halizai,*" Mt. 13:22. Uenyeji wetu uko Mbinguni, Wafilipi 3:20. Kwa hiyo ni lazima moyo wetu wa kupenda na nguvu zetu zote zikusanyike mahali pamoja penye makao yetu ya milele. Tumekumbushwa kuweka huba zetu kwa vitu vilivyoko juu na si kwa vitu vilivyo katika nchi, Kol. 3:2.

Kujishughulisha mno na vitu vya hapa na vya sasa vitakupinga na kukuondoa kwenye maendeleo ya tunzo ya Mbinguni.

III. **Kuwa na ushirika wa ndani na watu wasio mcha Mungu utakunyang'anya zawadi ya roho yako**.

Kuangalia pamoja na ufunuo hutueleza hivyo. "*msidanganyike, marafiki wabaya huharibu tabia njema*," 1 Kor. 15:33. *"heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakuketi barazani pa wenye mizaha,*" Zab. 1:1. Ni wazi ya kwamba hatuwezi kukosa kushirikiana na walimwengu. Kujaribu kufanya hivyo itatulazimisha kuuacha ulimwengu huu, 1 Kor. 5:9-11. Lakini tunaweza kuchagua wapenzi na washirika wetu kutoka kwa watoto wa mungu na wale walio na tabia njema yenye kupendelea mambo ya kiroho. Rafiki anayeweza kutuzuia tusifuate utakatifu anafaa kuachana naye kabisa. Lakini tuwatendee mema watu wote hata watenda dhambi, Gal. 6:10, na hakika lazima tuwafundishe (Biblia) injili, Mk. 16:15, 16. Bila kulegea katika kazi zetu hapa, ni lazima tujali sana kutunza roho zetu katika sehemu zile tulizozitaja.

IV. **Tuepukane na ugomvi na kushindana kuhusu yale ambao haidhuru**.

Mtume Paulo anatuonya "*...Kuwazia habari za maswali na mashindano ya maneno, ambayo, katika hayo hutoka husuda, na ugomvi na matukano, na shuku mbaya, na majadiliano ya watu walioharibika akili zao, waliokosa kweli, huku wakidhani ya kuwa utauwa ni njia ya kupata faida*, 1 Tim. 6:4, 5. Anasema, "*walakini uyakatae maswali ya upumbavu yasiyo na elimu, ukijua ya kuwa huzaa ugo,* 2 Tim. 2:2, 3. Anasihi sana tito akatae maswali ya upuzi, "*lakini maswali ya upuzi ujiepushe nayo, na nasaba, na ugomvi, na mashindano ya sheria. Kwa kuwa hayana faida, tena hayana maana,* Tit. 3:9. Kuna kitu cha uadui na chenye kuharibu tabia ya kiroho katika ugomvi mkali. Hatuwezi kukubali kuhatarisha imani yetu kwa vitu kama hivyo.

Mtu mwenye dini yenye msingi wa mawazo, wakati mwingi ataendeleza mawazo yake tu. Lakini yule mwenye dini yenye msingi wa neno la Mungu ataendeleza neno la Mungu na akizungumza kuhusu Bwana na Mbinguni na kazi yake kubwa itakuwa ni kuokoa roho zilizo potea. Ni jambo la kufurahia na zuri la kufahamu ya kwamba, wale wanaopenda kubishana sana kuhusu neno la Mungu ni wale wenye ufahamu hafifu kuhusu ukristo.

V. **Lazima tujihadhari na roho ya kiburi na dharau.**

Roho kama hii ni kuzuizi kikubwa kwa wokovu. Tumefundishwa kujifunga unyenyekevu. "*naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema,* 1 Pet. 5:5. Kiburi na uongo ni kizuizi kati ya mwanadamu na Mungu wake. Hutangua bidii yote ya kuwa mtakatifu. Kwa kweli Sulemani anatueleza ya kuwa Mungu anachukia wenye kiburi, "*kuna vitu sita anavyovichukia Bwana , naam viko saba vilivyo chukizo kwake, macho ya kiburi, ulimi wa uongo, na mikono imwagayo damu isiyo na hata,* Mith. 6:16, 17. Maombi ya Farisayo mwenye kiburi yalikuwa chukizo kwa Mungu, lakini mtoza ushuru mpole alishuka kwenda nyumbani kwake amehesabiwa haki kuliko yule, Lk. 18:9-14. Yesu aliweka mwongozo akisema, "*basi, ye yote ajinyenyekezaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni,"* Mt. 18:4. Na

tuombe kila siku msaada wa Mungu wa kufukuzilia mbali kiburi hiki cha uharibiru kutoka mioyoni mwetu na kujifunza unyenyekevu wa mtoto mdogo.

VI. **Moyo wa uvivu au uzembe utatuzuia safari yetu ya Mbinguni**.

Njia ya kwenda Mbinguni ni ya kupandisha. Yesu alisema lazima tukitendee kazi chakula kidumucho milele, Yn. 6:27. Imani bila matendo imekufa, Yak. 2:2. Mtu aliye mvivu katika maisha ya kawaida ataona ni vigumu kufanya kazi ya Mungu. Yesu alikufa ili kuwakomboa watu "*wale walio na juhudi katika matendo mema*," Tit 2:14.

VII. **Kutosheka na mambo ya msingi ya kwanza katika ukristo na kukataa chakula kigumu cha maisha ya kiroho na utumishi ni madanganyo ya hatari**.

Tusitosheke na kuwa watoto katika imani. Lengo letu liwe ni kufanyika watu wazima walio tayari kuwafundisha na wengine, Ebr. 5:12-14.

Tukitafakari haya, kitabu cha Waebrania kinatuhimiza "*kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu*," (6:1). Kujifunza ramani na kujua kuisoma kuhusu nchi fulani ya mbali si sawa na kwenda huko mwenyewe. Ni lazima tukue kila siku, "*...kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yetu Kristo...*" 2 Pet. 3:18. Kwa njia hiyo utakua katika wokovu, 1 Pet. 2:2.

Hakuna jambo muhimu zaidi kuliko kuokolewa kwa Roho zetu milele. Ili kupata lengo letu kuu hili, kila jitihada lazima zifanyike na kila kizuizi kiepukwe. Na sisi sote tuweke macho yetu kule kuliko makao yetu yenye upendo aliko Yesu na kukimbilia mbio mbele yetu kwa uvumilivu. Hakuna cho chote chenye thamani kinachoweza kugeuza mioyo yetu kando hata kwa muda mfupi.